

TANGAZO LA SERIKALI NA la tarehe

**SHERIA YA FEDHA SERIKALI ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)**

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu 6(1)(b)

**SHERIA NDOGO ZA (MABANGO NA MATANGAZO) ZA HALMASHAURI YA
MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016**

Jina 1. Sheria Nd\ogo hizi zitajulikana kama Sheria Nd\ogo za (Mabango na Matangazo) za Halmshauri ya Manispaa ya Lindi za mwaka 2016.

Matumizi 2. Sheria Nd\ogo hizi zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali na zitatumika ndani ya mipaka ya Halmashauri ya manispaa ya Lindi.

Tafsiri 3. Katika Sheria Nd\ogo hizi:-

“ada” maana yake ni tozo kwa mwombaji wa kibali kwa ajili ya kuruhusiwa kuweka bango au kutoa tangazo.

“afisa muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeoyote wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi aliyeulewa kusimamia sheria nd\ogo hizi.

“bango la tangazo” maana yake ni kitu kilichotengenezwa au kujengwa kwa kutumia kifaa chochote kwa ajili ya kutolea au kuweka tangazo ambacho ukubwa wake utapimwa kwa mita za mraba.

“kibali” maana yake ni idhini ya maandishi itolewayo na Mamlaka ili kuruhusu kujenga au kuweka bango au kutoa matangazo ambacho kitadumu kwa muda wa miaka mitatu au kadiri itakavyoelekezwa na Mamlaka.

“mamlaka” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

“maeneo maalum” maana yake ni maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya ofisi za Serikali, Taasisi, Mashirika ya umma yenye kuhitaji utulivu wakati wote au maeneo mengine ambayo Mamlaka itaona inafaa kwa nyakati tofauti.

"vibao au matangazo ya Biashara" maana yake ni kitu chichote kilichowekwa na wafanyabiashara kwa lengo la kutangaza biashara zao na ni pamoja na matangazo yaliyoandikwa au kubandikwa katika kuta, paa za nyumba na vyombo vya usafiri;

- Maeneo ambayo sheria hii haitatumika*
- 4. Sheria Ndogo hizi hazitatumika katika aina zifuatazo za matangazo.
 - (a) Mabango ya matangazo na mbao za matangazo yaliyopo ndani ya jengo na hayaonekani kwa nje;
 - (b) Mabango ya matangazo na mbao za matangazo yanayohusisha alama za usalama barabarani na alama za tahadhari za barabarani;
 - (c) Matangazo na mabango ya taasisi za Serikali na taasisi za kidini;
 - (d) Mabango na matangazo mengine ambayo mamlaka itaelekeza kwamba yasitozwe.
- Maombi ya Kibali*
- 5. Kila mwombaji wa kibali cha kuweka au kurekebisha bango la tangazo au ubao wa tangazo atalazimika kujaza fomu ya maombi kutoka Mamlaka kama ilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.
- Kibali cha matangazo*
- 6. -(1) Mtu, Kampuni au taasisi yoyote itaweka bango la tangazo au ubao wa tangazo baada ya kuomba na kupata kibali kutoka Mamlaka ikiwa ni pamoja na kulinia ada stahili kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.
 - (2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria ndogo hizi kitatumika hadi kufikia tarehe 30 ya mwezi Juni wa mwaka wa tatu bada ya kutolewa kibali hicho, baada ya hapo mwombaji anaweza kuomba kuhuishwa kibali chake kwa kufuata taratibu zote za maombi.
 - (3) Mamlaka haitatoa kibali cha mabango ya matangazo na mbao za matangazo endapo itabainika kwamba matangazo hayo yatachangia mmomonyoko wa maadili au yanashawishi kufanyika kwa matendo maovu au yanapingana na sheria za nchi na pia yanahatarisha usalama wa watu na mali zao.
 - (4) Mamlaka itatoa stika ambayo itabandikwa kwenye bango au ubao wa tangazo ambayo itaonesha namba ya kibali, jina la mmiliki, ukubwa wa bango au ubao, tarehe ya kuanza kutumika na kwisha kwa ada ya mwaka husika.
 - (5) vibali vitakavyotolewa chini ya sheria ndgo hizi vitalolewa na kusainiwa na

	Mkurugenzi au Mahandisi wa Manispaa.
<i>Kukubali au kutokubali kutoa kibali</i>	<p>7. -(1) Baada ya kupokea maombi ya kibali cha bango au tangazo Mamlaka itakuwa na uwezo wa kukubali au kukataa maombi husika kwa mujibu wa masharti yatakayoainishwa kwenye kibali.</p> <p>(2) Katika kushughulikia maombi hayo kipaumbele kitatolewa kwa mwombaji ambaye kumbukumbu zake zinaonesha kwamba anazingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Mamlaka.</p> <p>(3) Endapo maombi yatakataliwa mamlaka itamtaarifu mwombaji kwa maandishi ikimweleza sababu za kukataa maombi hayo.</p> <p>(4) Mamlaka itatoa kibali cha bango au ubao wa tangazo baada ya mmiliki wake kuwasilisha leseni ya biashara na/au usajiri wa biashara au jina la bishara.</p>
<i>Maeneo ya kuweka mabango na mbao za matangazo</i>	<p>8. -(1) Mtu yejote hataruhusiwa kuweka, kutundika, kubandika au kujenga bango au ubao wa tangazo katika eneo lolote lile kabla ya kibali cha maandishi cha Mamlaka.</p> <p>(2) Mtu yejote hataruhusiwa kubandika, kuchora, kuandika kwenye kuta au paa la jengo au sehemu nyingine ya jengo kabla ya kupata kibali cha Mamlaka.</p> <p>(3) Mamlaka itakuwa na uwezo wa kutoza ada za mabango na matangazo katika viwanja vya michezo au uzio wa muda katika maeneo ya ujenzi wa majengo na maeneo ya maegesho ya magari.</p>
<i>Muda wa kufanya promosheni</i>	<p>9. Mwombaji yejote atakayepata kibali cha kufanya promosheni atafanya kazi hiyo hadi ifikapo majira ya saa 4.00 usiku.</p>
<i>Majukumu ya mmiliki wa mabango na matangazo</i>	<p>10. -(1) Itakuwa ni jukumu la mwenye bango au tangazo kuhakikisha kwamba anasimamia na kutunza bango au tangazo lake katika hali nzuri na ya usalama katika kipindi chote cha kibali chake na pale ambapo muda wa kibali chake unapokwisha ni jukumu lake pia kuondoa bango au tangazo lake mara moja.</p> <p>(2) Ili kurahisisha mawasiliano kati ya Mamlaka au Wakala wake na mmiliki wa bango au tangazo, mmiliki wa bango au tangazo atahakikisha kwamba anaandika anuani ya Posta na ya makazi na namba zake za simu au barua pepe au utambulisho mwingine utakao idhinishwa na Mamlaka kwenye tangazo lake.</p>

- (3) Kila mmiliki wa bango kubwa atatakiwa kulilipia bima kwa madhumuni ya kutoa fidia kwa watu na mali zao watakaopata madhara kutokana na bango hilo.
- Wajibu wa mamlaka kusimamia na kuondoa mabango na matangazo*
- 11. –(1) Mamlaka itakuwa na uwezo chini ya Sheria ndogo hizi kusimamia, kuratibu na kudhibiti masuala yote yanayohusu mabango na matangazo.
 - (2) Mamlaka itakuwa na uwezo wa kuzuia, kuondoa au kubomoa bango au tangazo lolote ambalo litakuwa limewekwa au kujengwa kinyume sha Sheria Ndogo hizi kwa ghamama za mmiliki wa bango au tangazo.
 - (3) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mamlaka itakuwa na uwezo wa kumwagiza mmiliki wa bango au tangazo kuondoa, kubomoa au kutengeneza bango au tangazo lake kwa ghamama zake mwenyewe.
- Kutambulika kwa vibali vya awali*
- 12. Kibali chochote cha bango au tangazo ambacho kilitolewa kabla ya Sheria Ndogo hizi kutungwa na kuanza kutumika kitatambulika kama vile kimetolewa baada ya Sheria Ndogo hizi kuanza kutumika na kitadumu kwa kipindi chote cha miaka mitatu kuanzia tarehe, mwezi na mwaka wa kutolewa kibali hicho ikizingatiwa kwamba bango au tangazo hilo linatunzwa katika hali nzuri na ya usalama.
- Udhhibiti wa maeneo maalum*
- 13. Litakuwa ni jukumu la Mamlaka kuzuia uwekaji mabango au kufanya matangazo katika baadhi ya maeneo kwa madhumuni ya kuepusha bughudha na kero kwenye maeneo hayo.
- Alama za usalama barabarani*
- 14. –(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yeyote kuweka au kujenga bango au tangazo litakaloweza kuzuia au kusababisha alama za barabarani kutoweza kuonekana kwa urahisi na watumiaji wa barabara.
 - (2) Haitaruhusiwa kuweka bango au tangazo katika eneo la makutano ya barabara ambalo litazuia muonekano wa barabara na hivyo kusababisha adha kwa watumiaji wa barabara hizo.
- Uharibifu wa mali*
- 15. Mtu ye yeyote kwa uzembe au makusudi hataruhusiwa kuharibu mazingira na mali nyingine wakati wa kuweka, kujenga au kuondoa bango au tangazo lake.
- Urefu wa nguzo*
- 16. Nguzo za bango la tangazo au ubao wa tangazo zitakazojengwa au kuwekwa zitakuwa na urefu kama itakavyo elekezwa na Mamlaka.
- Mabango na matangazo katika*
- 17. Ili kuepuka maadhara kwa watumiaji wengine wa barabara mabango na matangazo yote yatakayowekwa au kutundikwa kwenye vyombo vya usafiri

<i>vyombo vya usafiri</i>	kama vile magari na pikipiki za magurudumu mawili na magurudumu matatu hayatajitokeza pembezoni mwa vyombo hivyo vikiwa katika mwendo.
<i>Viwango vya Ada ya mabango na matangazo</i>	18. Mamlaka itaweka viwango vya ada ya mabango na matangazo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.
<i>Matangazo ya kibashara ya muda mfupi</i>	<p>19. –(1) Mmiliki yoyote wa tangazo la muda mfupi la biashara ataruhiwa kutangaza biashara yake baada ya kuomba na kupata kibali cha kutangaza biashara yake kutoka kwa mamlaka na kulipia ada ya matangazo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Tangazo fupi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo hii ni pamoja na matangazo mbalimbali ya kijamii ambayo mmiliki wake hapewi kibali cha matangazo cha miaka mitatu na kitadumu kwa muda ambaa mamlaka itaelekeza mara kwa mara.</p>
<i>Uwezo wa kufanya ukaguzi</i>	20. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi katika jengo, mabango au eneo lolote kwa madhumuni ya udhibiti na usimamizi wa mabango na matangazo chini ya Sheria Ndogo hizi.
<i>Kufifilisha kosa</i>	21. Mkurugenzi wa Halmashauri anaweza kufifilisha kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, iwapo mkosaji atakuwa amekiri kwa maandishi na atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini tu.
<i>Adhabu</i>	22. Mtu ye yeyote atakayekwenda kinyume cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Elfu Hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI

[*Chini ya kifungu cha 5*]

Sehemu "A"

Halmashauri ya Manispaa ya

*Ninaomba/tunaomba kibali cha *kujenga/kuweka/kutoa bango au Ubao wa tangazo.

NA.	TAARIFA ZA MWOMBaji
1.	Jina na anuani ya mwombaji
2.	Nambari ya simu ya mwombaji
3.	Eneo analokusudia kuweka bango au tangazo
4.	Namba ya Kiwanja na Kitalu anapokusudia kuweka bango au tangazo
5.	Aina ya bango au tangazo linalokusudiwa kuwekwa au kutolewa
6.	Muda wa bango au tangazo
7.	Ukubwa wa bango/tangazo
8.	Bango ling'aalo au kubadilisha tangazo/lisilong'aa.
9.	Namba ya leseni ya biashara
10.	Jina la Biashara

Saini ya mwombaji: Tarehe:

Sehemu "B" (*kwa matumizi ya ofisi tu*)

1. Maombi Na.
2. Ada ya kibali Sh.
3. Naamba ya stakabadhi ya malipo:
4. Tarehe:

Maoni ya Muidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali.

Sababu:.....
.....
.....

Jina:

Saini:

Tarehe:

* Futa isiyotakiwa.

JEDWALI LA PILI

KIBALI CHA BANGO/TANGAZO

[Chini ya kifungu cha 6(1)]

1. Jina kamili la mwombaji:
.....
2. Anuani ya mwombaji:
.....
3. Nambari ya kiwanja na kitalu:
.....
4. Kata ya
.....
5. Barabara/mtaa:
.....

6. Aina ya bango/tangazo:

.....

7. Ukubwa wa bango/tangazo:

.....

8. Masharti ya kibali:-

(a)

.....

.....

(b)

.....

.....

(c)

.....

.....

(d)

.....

.....

(e)

.....

.....

(f)

.....

.....

9. Kibali hiki kitatumika kuanzia tarehe mwezi
mwaka 20..... na ukomo wake wa kutumika ni tarehe
mwezi mwaka 20.....

Kibali hiki kimetolewa leo, tarehe mwezi mwaka 20.....
na:-

Jina kamili:

Cheo: Saini:

JEDWALI LA TATU

VIWANGO VYA ADA YA MABANGO NA MATANGAZO

[Chini ya kifungu cha 18]

NA	BANGO/TANGAZO	KIWANGO CHA USHURU
1	Mabango yenyne mwanga.	100,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka
2	Mabango yasiyo na mwanga.	80,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka
3	Mabango ya kielektroniki.	120,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka
4	Bango linalowaka na kubadilisha matangazo ya watu au makampuni tofauti.	150,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka
5	Matangazo kwenye kuta/paa la nyumba.	60,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka
6	Matangazo mengine ya karatasi.	15,000/= kwa mita ya mraba kwa siku
7	Matangazo kwa kutumia gazebo au miamvuli.	5,000/= kwa mita ya mraba kwa siku
8	Matangazo kwa kutumia vitambaa kwa mita moja ya mraba.	6,000/= kwa siku moja
9	Matangazo kwa kutumia vyombo vya usafiri na vipaza sauti.	100,000/= kwa siku moja
10	Promosheni za makampuni, taasisi au mashirika.	150,000/= kwa siku moja.

JEDWALI LA NANE

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA (Chini ya kifungu cha 22)

Mimi wa S.L.P.
niayefanya biashara ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, nakiri kutenda kosa la ikiwa ni kinyume na kifungu cha cha Sheria ya Ndogo za (Masoko na Uvuvi) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za Mwaka 2016. Kwa hiyo, kwa hiaria yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yejote nakubali kulipa faini ilioainishwaa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliopewa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini:

Mbele yangu:-

Jina:

Saini:

Wadhifa:

Sheria ndogo hizi zilipigwa Muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kufuatia maamuzi yaliyopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 28 mwezi Aprili, 2016 mbele ya:-

J. M. Satura,
Mkurugenzi wa Manispaa.

Mohamed L. Lihumbo,
Mstahiki Meya wa Manispaa.

NAKUBALI

Dodoma

John Pombe Magufuli,
RAIS.

Tarehe:.....